





Fasihi *na* Masuala Ibuka



Kwa Heshima ya Marehemu Prof. Ken Walibora



Wahariri

Mosol Kandagor
John Kobia
Iribe Mwangi
Leonard Chacha Mwita
Fred Simiyu Wanjala

ASIHI NA MASUALA IBUKA

wa Heshima ya Marehemu Prof. Ken Walibora

Wahariri

Mosol Kandagor

John Kobia

Iribe Mwangi

Leonard Chacha Mwita

Fred Simiyu Wanjala

© Mosol Kandagor, John Kobia, Iribe Mwangi, Leonard Chacha Mwita,
Fred Simiyu Wanjala.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupigisha chapa,
kutafsiri au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini, kwa maandishi
ya waandishi.

Chapa ya kwanza 2025.

ISBN 978-9914-37-604-3

Kimechapishwa na RealText Publishers Ltd.

Barua pepe: realtext15@gmail.com

WASIFU WA WAANDISHI

Joseph Nyehita Maitaria

Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Karatina

Pamela M.Y. Ngugi

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

Pius Nyakundi

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

Mary K. Njeru

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Chuka

John M. Kobia

Profesa katika Chuo Kikuu cha Chuka

Dorcas Musyimi

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Chuka

Beverlyne Asiko Ambuyo

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Maseno

Clara Momanyi

Profesa, Mtafiti na Mwandishi wa Kiswahili

Fred Wanjala Simiyu

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Kibabii

Ogonda Samuel Sinzore

Mzamili katika Chuo Kikuu cha Maseno

Deborah Nanyama Amukowa

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Maseno

Musembi Nzilani Naomi

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga

Justus Kyalo Muusya

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

Aidah Mutenyo

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Kabale

Roseline Mwikali Kasuma

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Rongo

Mark A. Odawo

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Rongo

Edwin Masinde

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

Lucy Wanyela

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

Evans M. Mbuthia

Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Nairobi

Zachary Njagi Ndwiga

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Embu

Nyandwaro K. Lena

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Rongo

Benard Odoyo Okal

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Maseno

Marolyne Jerujael Moses

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Rongo

Mosol Kandagor

Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Moi

YALIYOMO

WASIFU WA WAANDISHI	iii
DIBAJI	vii

SURA YA KWANZA

Fasihi kama Chombo cha Kubainishia Mielekeo ya Watu Kuhusu Lugha: Mifano Katika Riwaya ya <i>Kidagaa Kimemwozea</i> (Ken Walibora, 2012) <i>Joseph Nyehita Maitaria, Pamela M. Y. Ngugi na Pius Nyakundi</i>	1
--	---

SURA YA PILI

Mchango Wa Ken Walibora Katika Mshikamano Wa Kitaifa: Tathmini Ya <i>Kufa Kuzikana</i> <i>Mary K. Njeru, John M. Kobia na Dorcas Musyimi</i>	15
--	----

SURA YA TATU

Maudhui ya Ubaguzi Katika Diwani ya <i>Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine</i> (Walibora, K. & Mohamed, S.A., 2007) <i>Beverlyne Asiko Ambuyo</i>	29
---	----

SURA YA NNE

Ushairi kama Chombo Cha Kufasiria Siasa za Juzi, Jana na Leo Nchini Kenya: Nafasi ya Utungo wa <i>Tarbia Pwani na Bara</i> <i>Clara Momanyi</i>	43
---	----

SURA YA TANO

Dhana ya Kifo katika Mashairi Pepe ya Kumwomboleza Ken Walibora Kwenye Kumbi za Kulikoni za Wataalam wa Kiswahili <i>Fred Wanjala Simiyu</i>	63
--	----

SURA YA SITA

Taswira ya Mwanamke Kiongozi Katika Tamthilia za <i>Pango</i> (Wamitila, 2003) na <i>Kigogo</i> (Kea, 2016) <i>Ogonda Samuel Sinzore, Deborah Nanyama Amukowa na Beverlyne Asiko Ambuyo</i>	79
---	----

SURA YA SABA

Fasihi za Kiitikadi na Mchango Wake Katika Jamii ya <i>G. K Mkangi</i> <i>Naomi Nzilani Musembi na Mosol Kandagor</i>	93
--	----

SURA YA NANE

Kifungo kama Mkakati wa Kudhibiti Jamii Katika Riwaya za Ken Walibora <i>Justus Kyalo Muusya</i>	107
---	-----

SURA YA TISA

Nguzo Mama: Mfano wa Kazi Teule za Ken Walibora Kama Fasili Bora ya Maisha Yake

Aidah Mutenyo na Mosol Kandagor 121

SURA YA KUMI

Udumishaji Tabaka Kama Kichocheo cha Ufyefye wa Maadili ya Kielimu Katika Riwaya Teule za Ken Walibora

Roseline Mwikali Kasuma na Mark A. Odawo 129

SURA YA KUMI NA MOJA

Mchango wa Ken Walibora Waliaula Katika Maendeleo ya Taaluma na Jamii

Edwin Masinde na Lucy Wanyela 149

SURA YA KUMI NA MBILI

Nafasi ya Kiswahili Katika Uangamizaji wa Ubeberu wa Kitamaduni

Evans M. Mbuthia na Zachary Njagi Ndwiga 161

SURA YA KUMI NA TATU

Nafasi ya Nyimbo za Kizazi Kipya Katika Kufundisha Masuala Mtambuko Katika Mtaala wa Umilisi

Nyandwaro K. Lena 171

SURA YA KUMI NA NNE

Udadavuzi wa Hadithi Fupi ya *Damu Nyeusi* ya Ken Walibora Kwa Msingi wa Nadharia ya Uasililia

Benard Odoyo Okal na Marolyne Jerujael Moses 187

SURA YA PILI

Mchango Wa Ken Walibora Katika Mshikamano Wa Kitaifa: Tathmini Ya Kufa Kuzikana

Mary K. Njeru, John M. Kobia na Dorcas Musyimi

IKISIRI

Kuwepo kwa mshikamano wa kitaifa husaidia katika kukuza ushirikiano wa kimaadili na kuandaa nafasi za kimaisha kwa kila mtu katika taifa lolote lile. Nchini Kenya, kumekuwa na mizozo mingi kwa misingi ya kikabila ambayo kwa muda mrefu imetishia kuvuruga mshikamano wa kitaifa. Fasihi ni chombo ambacho kinaweza kutumiwa kujenga msingi wa utu, usawa, upendo na usalama wa watu katika jamii. Makala hii inakusudia kuangazia jinsi ambavyo mwandishi Ken Walibora amesawiri mshikamano wa kitaifa, kuonyesha chanzo cha mizozo katika jamii, juhudi za kuleta mshikamano na changamoto za kuleta mshikamano huo. Makala hii itaongozwa na nadharia ya uhalisia iliyoasisiwa katika Karne ya 19 na E. Goffman. Kwa mjibu wa nadharia hii, mwandishi husukumwa na nia ya kuusawiri uhalisia katika ukamilifu na wakati wake maalum. Riwaya ya Kufa Kuzikana (Walibora, 2003) iliteuliwa kimakusudi kwa kuwa maudhui yake makuu yanahusiana moja kwa moja na mada ya makala hii. Kazi hii ni muhimu katika kuthibitisha kuwa fasihi ya Kiswahili inatekeleza dhima muhimu katika kuhamasisha jamii kuhusu haja ya kuwepo kwa mshikamano wa kitaifa.

UTANGULIZI

Mshikamano wa kimataifa ni ushiriki wa kila mmoja katika mchakato wa kufanya maamuzi ya pamoja, na kwa namna ya pekee kutambua kanuni ya ushirikishaji wajibu (Nyanda, 2017). Zaidi ya hayo, Nyanda anasisitiza kutokomeza kabisa mizizi ya utengano, uonevu, umaskini na ukosefu wa usawa na uwiano kati ya mataifa. Aidha, anasisitiza kuwa mtazamo na utendaji wa namna hii ndio unaoweza kuleta amani, usalama na maendeleo, ikiwa ni pamoja na utetezi wa haki msingi za binadamu.

Katika historia ya Kenya, kumeshuhudiwa mizozo mingi kwa misingi ya kikabila. Kwa mfano mwaka wa 1992 eneo la Molo, 1997 eneo la Likoni katika kaunti ya Mombasa, 2005 katika Mlima Elgon na vilevile mwaka wa 2014 eneo la Mpeketoni kaunti ya Lamu (Nyiri, 2014). Isitoshe, kuzuka kwa ghasia za baada ya uchaguzi mkuu nchini Kenya mwaka wa 2007 hadi 2008 hasa baada ya matokeo ya kura za urais kuliashiria kuwepo kwa farakano la muda ambalo halikuwa limeshughulikiwa kwa muda mrefu. Mizozo hiyo ilirudisha nyuma maendeleo ya Kenya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hii

ilitokana na mambo mbalimbali kama vile watu kuuawa huku wengine wakiachwa bila makao, maelfu ya watoto wa umri wa kwenda shule kutimuliwa na baadhi yao wakatoka shule kwa sababu ya ukosefu wa karo, uhaba wa chakula, ukosefu wa usalama, kuathiriwa kwa shughuli za kilimo, unyakuzi wa ardhi, kukatizwa kwa uchukuzi na mawasiliano na uharibifu wa mali na mazingira.

Serikali ya Kenya imetumia mikakati mbalimbali ili kuimarisha mshikamano wa kitaifa. Mojawapo ya mikakati hiyo ni kuundwa kwa Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (NCIC) iliyoanzishwa chini ya sheria Na. 12 ya 2008 ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa. Hii ni mojawapo ya Tume za Ajenda ya Nne zilizobuniwa kutokana na Makubaliano ya Amani ya Kitaifa. Kwa mujibu wa Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Masuala ya Kikatiba (2012), jukumu kuu la tume hiyo ni kuchangia katika kuendeleza usawa wa nafasi, mahusiano mema, upatanifu na kuishi kwa amani na umoja miongoni mwa watu wa makabila na rangi mbalimbali nchini Kenya, pamoja na kuishauri serikali, yakiwemo mapendekezo na uwezekano wa kuingilia kati ili kurekebisha hali.

Katiba ya Kenya (2010) inatoa mazingira bora kwa raia wote kuishi kwa maelewano, ambapo sura ya nne inahusu sera, sheria na muundo wa uwiano na utangamano wa kitaifa. Kwa hivyo, inatoa maelezo ya jinsi ya kuboresha uwiano na utangamano wa kitaifa. Mbali na katiba, uundaji wa sera na miongozo mbalimbali ni hatua muhimu katika kuleta mshikamano wa kitaifa. Sera na miongozo hiyo ni pamoja na sera ya kitaifa ya ardhi na ile ya kuleta amani na kusuluhisha mizozo.

Fasihi ni kielelezo cha hali halisi katika jamii. Njogu (1997) anasisitiza kuwa fasihi ni amali ya jamii ambapo msanii anachukuliwa kama mmoja katika jamii na mwenye nafasi yake katika jamii hiyo. Kwa hivyo, fasihi ina jukumu kwa jamii katika kiwango cha mtu binafsi na vilevile kiwango cha jamii kwa jumla. Aidha, Wellek na Warren (1954) wanadai kuwa fasihi hueleza jamii kwa msingi kuwa 'Fasihi ni kioo cha jamii'. Kutokana na msingi wa maelezo hayo, makala hii inalenga kuangazia jinsi ambavyo mwandishi Ken Walibora amesawiri mshikamano wa kitaifa, kuonyesha juhudi za kuleta mshikamano na changamoto za kuleta mshikamano huo katika riwaya ya *Kufa Kuzika* (Walibora, 2003).

Dhana ya Mshikamano wa Kitaifa

Mshikamano wa Kitaifa unahusisha umoja, usawa, uhuru, demokrasia, kutokuwa na vita, kuwepo na amani, haki ya kijamii na kuzingatia kanuni za kisheria. (Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Masuala ya Kikatiba, 2012). Aidha, kuwepo kwa mshikamano wa kitaifa husaidia katika kukuza ushirikiano miongoni mwa wanajamii, kujenga amani kwa makundi ya kikabila, kudhibiti hali ya mafarakano na kuimarisha desturi ya kuheshimu

thamani ya maisha ya binadamu. Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN, 2013), mshikamano ni msingi wa maadili ya kimataifa ya kuisitiza mahusiano ya watu katika karne ya 21. Hata hivyo, moja ya vikwazo vikubwa vya mshikamano na utangamano ni ukabila.

Makala hii iliongozwa na nadharia ya Uhalisia. Nadharia hii iliasisiwa katika karne ya 19 na kufafanuliwa zaidi na E. Goffman aliyeishi kati ya mwaka (1922- 1982). Baadhi ya wataalamu wengine wanaotoa mchango wao ni Gustav Flaubert (1846-1854), George Lukacs (1963), Rene Wellek (1960), Macdowall Arthur (1918) na Hegel G. (1979). Lukacs (1963) anaeleza kuwa mwandishi anasukumwa na njia ya kuusawiri uhalisia katika ukamilifu na wakati wake maalumu. Mwandishi anapaswa kupenya chini ya picha za kijuujuu na kudhihirisha mifanyiko ya mabadiliko yaliyopo. Uhalisia wa maisha katika jamii unapewa msingi mkubwa wa uandishi kuhusu uhalisia. Tukio, mhusika au mandhari huelezwa kama vya kihalisia ikiwa vinafanana na sura fulani ya maisha.

Wamitila (2002) anaeleza kuwa uhalisia unasisitiza usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Waaandishi wa kazi za kihalisia wanatoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii ya mwandishi anayehusika. Aidha, Fasihi yoyote lazima ionekane kama kioo cha jamii. Hivyo basi, lazima jamii iweze kujitazama na kujiona kupitia fasihi ambayo ni zao la jamii. Msingi wa nadharia hii ni kuwa sanaa iwakilishe ukweli na kuwakilishwa kwa maneno halisi, iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira. Kutokana na maelezo hayo, nadharia ya Uhalisia ilisaidia katika kuangazia jinsi ambavyo Walibora katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* amesawiri uhalisia wa hali ya mshikamano wa kitaifa hasa nchini Kenya kwa kuonyesha jitihada za kuleta mshikamano na vilevile changamoto katika kuleta mshikamano wa kitaifa.

Makala hii inaongozwa na mihimili ifuatayo:

- (a) Kazi ya fasihi inajitosheleza. Kazi ya sanaa sharti iwe na msuko, mtindo, wahusika na ujumbe.
- (b) Kazi ya msanii inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira yake. Uhalisia sharti ujihusishe na mambo halisi yanayotokea katika mazingira halisi kupitia kwa wahusika.
- (c) Wahusika ni vielelezo yakini vya binadamu wa kawaida kwa vile wao hutumia lugha ya binadamu wa kawaida. Hali halisi ya wahusika na lugha wanayoitumia humwezesha mwanadamu kujifafanulia uwezo wake wa kutenda mambo na mtazamo wake kuhusu maisha.
- (d) Msanii anaangazia matatizo na kuchunguza chanzo chake. Anachunguza mabadiliko ambayo hutokea kwa kipindi fulani cha historia na kuyatumia kuwasawiri wahusika wake.

Kumhusu Ken Walibora, Mwandishi wa *Kufa Kuzikana*

Ken Walibora alizaliwa tarehe sita Januari mwaka wa elfu moja mia sita tisini na nne Baraki kaunti ya Bungoma kisha wakahamia Kitale na baadaye Cherangani. Baada ya kuhitimu masomo ya shule ya upili, alianza kufundisha Kiingereza na Kiswahili katika shule za sekondari halafu akajiunga na taasisi ya Kenya ya Utawala alikosomea maendeleo ya kijamii. Baadaye akawa afisa wa majaribio kwa miaka minane, na kutoka hapo akajiunga na shirika la utangazaji la Kitaifa (KBC) alifanya kazi kwa miaka mitatu. Akiwa katika KBC alijiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi ambapo alisomea Kiswahili na fasihi. Baada ya kufanya kazi Nation Media Group kwa muda alienda Marekani ambapo alisomea Fasihi linganishi hadi kiwango cha Ph.D. na kuanza kufunza Chuo Kikuu cha Wisconsin Madison kwa takriban miaka minne. Baadaye alirejea nchini Kenya katika kampuni ya Nation Media Group ambapo alisimamia masuala ya viwango vya ubora wa Kiswahili. Hadi kifo chake, Ken Walibora alikuwa mkurugenzi wa kituo cha masomo ya masuala ya ulimwengu na lugha pamoja na kuwa mhadhiri katika kitivo cha mahusiano ya kimataifa na diplomasia Chuo Kikuu cha Riara.

Ken Walibora alitamba katika nyanja zote za fasihi ya Kiswahili na kupita mipaka yake. Ni mtunzi wa riwaya, mashairi, hadithi fupi, fasihi ya vijana na fasihi ya watoto. Kwa ushirikiano na S A Mohamed, wametunga *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* (2006). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* na *Tumbo Lisiloshiba* ni miongoni mwa hadithi fupi zake zilizochapishwa na kuteuliwa kusomwa na kutahiniwa katika shule za sekondari nchini Kenya. Baadhi ya riwaya alizooandika ni *Siku Njema* (1996), *Kufa Kuzikana* (2003), *Kidagaa Kimemwozea* (2012), *Upande Mwingine* (2009) na *Ndoto ya Amerika* (2001). Vilevile, amehusika katika fasihi ya watoto kupitia vitabu kama vile *Ndoto ya Almasi* (2012), *Chapuchapu* (2012), *Pepela na Mto* (2012), *Bobby the Dog* (2013), *Hazina Bora* (2012) na *Innocent Long Lost* (2005). Katika utanzu wa Ushairi, ameandika mashairi katika diwani ya *Waja Leo* (2012) pamoja na kutunga tawasifu yake ya *Nasikia Sauti ya Mama* (2014). Kando na utunzi, ameandika kazi nyinginezo kama vile *Narrating Prison Experience: Human Rights, Self, Society and Political. Incarceration in Africa* (2013). Isitoshe, kwa miaka mingi amejihusisha katika uandishi wa makala pamoja na uhakiki wa kazi mbalimbali.

Uchambuzi wa Riwaya ya *Kufa Kuzikana*

Riwaya ya *Kufa Kuzikana* iliandikwa na mwandishi Ken Walibora. Ni kazi ya kiubunifu inayotokea katika nchi ya Kiwachema, ambapo makabila mawili yanazozana; Wakanju na Wakoroshu. Licha ya Akida na Tim kutoka katika makabila tofauti yenye uadui, wanapendana na kufaana katika kila jambo. Wao ni marafiki wa kufa na kuzikana licha ya migogoro, migongano, vikwazo na vizingiti katika uhusiano wao.

Licha ya hadithi hii kuwa ya kiubunifu, inasawiri hali halisi katika nchi nyingi Barani Afrika ambapo watu wasio na hatia wanauawa kinyama kwa sababu ya uhasama wa kikabila. Kwa mfano, mauaji ya halaiki nchini Rwanda mwaka wa 1994 ambapo watu takriban elfu mia nane waliuawa na Wahutu waliolenga watu wa jamii ya Watutsi. Nchini Kenya, mizozo ya kikabila imeshuhudiwa mara kwa mara tangu kupatikana kwa uhuru hasa miaka ya tisini sehemu za Magharibi. Zaidi ya hayo, Mzozo wa 1990 nchini Kenya maarufu kama 'Saba saba' ulishuhudiwa ambapo watu wengi waliangamia. Vilevile, mzozo wa baada ya uchaguzi mkuu wa 2007 hadi 2008 ulikuwa wa kihistoria nchini Kenya. Watu katika maeneo ya Magharibi, Bonde la Ufa na Pwani walipoteza maisha yao huku wengine wakiachwa bila makao. Hivyo, ni wazi kwamba Ken Walibora alitunga riwaya ya *Kufa Kuzikana* kutokana na hali halisi aliyoshuhudia katika jamii yake.

Katika uchambuzi wa riwaya ya *Kufa Kuzikana*, vipengele vitakavyozingatiwa ni pamoja na; chanzo cha mizozo katika jamii, jitihada za mshikamano wa kitaifa na changamoto za mshikamano wa kitaifa.

Chanzo cha Mizozo katika Jamii

Katika jamii yoyote ile, mizozo inaweza kutokea kwa sababu mbalimbali, jambo ambalo hutishia mshikamano na uwiano katika jamii husika. Walibora katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* amesawiri vyanzo vya mizozo kama ifuatavyo:

Ardhi

Katika mataifa mengi hasa Barani Afrika, mizozo ya ardhi imekuwa dhahiri na kusababisha madhara mengi. Mojawapo ya chanzo cha mizozo ya ardhi ni mipaka ya mashamba kama inavyojitokeza katika kifungu kifuatacho:

Nilimwonyesha baba karatasi ile akatua kitambo na kusema, "Mwanangu tangu mdogo nimevisikia vitisho hivi. Vishindo vya mashua havishtui bahari." Mzee Zablon, babake sahibu wanguTim, alikuja kwetu siku hiyo. Alikuwa ni mkorosho. Shamba lake lilipakana na letu. **Mara mbili tatu wamegombana na baba juu ya mpaka wa shamba.** lakini hawakuwa na uhasama mkubwa sana kati yao.

(*Kufa Kuzikana*, uk 5-6.)

Kutokana na kifungu hiki, mizozo ya ardhi huzuka watu wanapozozana kuhusu mipaka ya mashamba. Jambo hili linadhihirika kupitia mhusika Akida anayeeleza kuwa baba yake na Mzee Zablon walizozana mara kwa mara kuhusu mipaka ya mashamba kwani yalipakana. Hata hivyo, Akida anaeleza kuwa licha ya kuzozania mipaka ya mashamba yao, hapakuwa na uhasama mkubwa sana kati ya baba yake na Mzee Zablon.

Siasa

Sababu nyingine ya kuwepo kwa mizozo katika jamii ni uchochezi unaotokana na wanasiasa na watu wengine wenye ushawishi mkubwa serikalini. Haya yanadhibitika kupitia kifungu kifuatacho:

. . .wadadisi wa mambo wanasema, ingawa makabila hayo mawili yamekuwa na chuki baina yao, **huenda vita hivyo vimechochewa na watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa.** Mapema wiki hii wahariri wakuu wa magazeti mawili nchini Kiwachema walitiwa nguvuni baada ya kuchapisha habari za vita hivyo. (*Kufa Kuzikana*, Uk 61)

Kutokana na dondoo lililotolewa, mizozo katika jamii hutokana na uchochezi wa viongozi wa kisiasa na pia watu wenye ushawishi mkubwa serikalini. Kwa mfano, Walibora katika Kufa Kuzikana anaeleza kuwa hata ingawa makabila ya Wakanju na Wakoroshio yalikuwa na chuki baina yao, **huenda mizozo iliyokuwa Wilayani Koroshio ilichochochewa na watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa.** Aidha, ukweli wa jambo hili unadhihirika kupitia matamshi haya:

Mzee Zablon, babake sahiibu wangu Tim, alikuja kwetu siku hiyo. Alikuwa Mkoroshio. Shamba lake lilipakana na letu. Mara mbili tatu wamegombana na baba juu ya mpaka wa shamba, **lakini hawakuwa na uhasama mkubwa sana kati yao. Nakumbuka walivyoandamana pamoja kwenda kwenye madarasa ya ngumbaru, mikutano ya hadhara na hamkani nyingine.** “Ndugu yangu Sululu umeyasikia? Ilani imesambazwa kote Koroshio kwamba Wakanju wahame.” (*Kufa Kuzikana*, uk 5- 6)

Dondoo la hapo juu linaonyesha kuwa, kabla ya mbegu ya chuki kupandwa na wanasiasa katika jamii, watu wa makabila mbalimbali waliishi kwa amani na utangamano. Hii ndiyo maana Mzee Zablon na Sululu katika *Kufa Kuzikana* waliokuwa wa makabila tofauti wanatembeleana na kuandamana pamoja kwenda kwenye madarasa ya ngumbaru, mikutano ya hadhara miongoni mwa shughuli zingine. Kwa mujibu wa Kimenyi na Ndung'u (2005), mizozo ya ardhi katika eneo la Bonde la Ufa mwaka 1992, 1997, 2002 na 2007 hadi 2008 ilichochochewa na Wanasiasa nchini Kenya hasa wakati wa uchaguzi mkuu. Muchiri (2016) anaafikiana na madai hayo kwa kusema kuwa watu ambao wanapaswa kuwaongoza na kuwaelekeza Wakenya ndio hutumia matamshi ya uchochezi huku wakiwatumia vijana kueneza chuki dhidi ya wale wanaodhaniwa kuwa `wageni` miongoni mwao. Kwa hivyo, inadhibitika kuwa miongoni mwa vyanzo vya mizozo katika jamii ni uchochezi wa watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa.

Ukabila

Tofauti za kikabila huzua mizozo katika jamii. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, Walibora anashadidia kauli hii kwa kuonyesha kuwa kuna uhusiano wa karibu baina ya mizozo na ukabila. Kwa mfano:

...siku moja mbunge wa kwetu Johnstone Mabende alihutubia Mkutano wa Hadhara katika kituo cha biashara cha Baraki. Nakumbuka mpaka sasa alivyosema: **“hatutaki `madoadoa`hapa. Wakanju sharti wahame warudi kwao Kanju.”** mheshimiwa Mabende alishangiliwa kwa hoihoina nderemo na Wakorosho.

(*Kufa Kuzikana*, uk 2)

Kupitia dondoo lililonukuliwa, tunaeleza kisa ambapo mbunge Mabende alihutubia watu huko Baraki na kusema kuwa hawakutaka `madoadoa`. Aliwataka Wakanju wahame warudi kwao Kanju. Hii inaonyesha matumizi ya matamshi ya chuki na uchochezi kwa misingi ya kikabila kutokana na wanasiasa dhidi ya watu ambao hawakuwaunga mkono kisiasa kwa manufaa yao wenyewe. Vilevile, chuki iliyokithiri dhidi ya makabila tofauti inajitokeza katika mfano ufuatao:

Nyie Wakorosho na sisi Wakanju ni ndugu, Meno ya mbwa hayaumani...**sisi Wakorosho tumekuwa tukifanya shinikizo nyie Wakanju mtoke Wilaya ya Korosho...tangu mdogo nikisikia**, Wakanju ni walowezi Watimuliwe warudi kwao
(*Kufa Kuzikana*, Uk 29)

Walibora anamtumia mhusika Tim ambaye ni rafiki wa kufa na kuzikana wa Akida licha ya kuwa wao ni wa makabila tofauti tofauti. Vita vya kikabila vinapozuka wilayani Korosho, wanahofia kwamba mambo huenda yakawa mabaya zaidi, ndiposa Tim anamwambia Akida kuwa wao Wakorosho wamekuwa wakifanya shinikizo Wakanju watoke wilaya ya Korosho, mambo ambayo amekuwa akiyasikia tangu akiwa mdogo. Kwa mujibu wa Chachali (2008), tofauti za kikabila na kidini ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vya machafuko sehemu mbalimbali duniani hususan barani Afrika. Anaendelea kusema kuwa tofauti hizo hustawi vizuri zaidi mahala ambapo kuna manung'uniko kuhusu haki na usawa hasa katika uchumi. Kwa hivyo ni wazi kwamba hisia za kikabila huchangia pakubwa katika kusababisha mizozo katika jamii, jambo ambalo ni tishio kubwa katika mshikamano wa kitaifa.

Jitihada za Mshikamano wa Kitaifa

Katika *Kufa Kuzikana*, Walibora amesawiri juhudi za kuleta mshikamano wa kitaifa kwa namna mbalimbali. Miongoni mwa jitihada hizo ni:

Mahusiano Thabiti na Bora

Mahusiano thabiti na bora baina ya watu kutoka kwenye tamaduni mbalimbali ni muhimu katika mshikamano wa kitaifa. Katika *Kufa Kuzikana*, kifungu kifuatacho kinashadidia:

...makabila yetu yana hasama ya jadi, kila moja likijifutua na kubeua jingine. **Kinyume cha yote haya Tim nami tukiitana “shemeji”;** mtu afasiri atakavyo, kwetu mamoja. **Hatukuwa na shaka juu ya dhati ya urafiki wetu. Naam urafiki wa *Kufa Kuzikana* hasa.** (*Kufa Kuzikana*, uk 8)

Kutokana na dondoo lililotolewa, Akida anakiri kuwa makabila yao na Tim yalikuwa na uhasama wa jadi uliokithiri. Hata hivyo, yeye na Tim walikuwa na urafiki wa dhati wa tangu wakiwa wachanga. Wao walipendana na kufaana katika kila jambo bila kuathiriwa na hisia za kikabila. Vilevile, kiwango cha urafiki wa dhati baina ya Akida na Tim kinajitokeza kupitia dondoo hili:

“...umefutwa kazi kwa ajili yangu?” “usijali Akida,” Tim alinihakikishia. **“Yetu mamoja, ije heri au shari. Siwezi kukulaumu katu.** Sasa nahofia tu familia yangu na babako. Sijui hali zao.” (*Kufa Kuzikana*, uk 65)

Tim anafutwa kazi na mjombake kwa kumlaumu kwamba anasaliti kabila lao la Wakoroshu kwa kushirikiana na Akida ambaye ni Mkanju na kumweka nyumbani kwake Shauri Moyo. Licha ya kukabiliwa na uhalisia wa kufutwa kazi na hatimaye tishio la hali ngumu ya maisha, Tim anakuwa tayari kwa vyovyote vile kudumisha urafiki wake na Akida. Kupitia urafiki wa kufa na kuzikana baina ya Akida na Tim, Walibora anathibitisha kuwa kuna uwezekano wa watu kudumisha uwiano na mshikamano wa kitaifa kwa kutupilia mbali tofauti za kitamaduni na kikabila miongoni mwa watu katika taifa. Kwa hivyo, kuna uwezekano mkubwa wa wanajamii kuwa na uwiano pale ambapo watu wenye misingi tofauti ya kikabila na kitabaka wanashirikiana kila mara.

Nafasi Sawa za Maisha

Kuwepo kwa nafasi sawa za maisha baina ya watu walio na tamaduni tofauti tofauti. Katika *Kufa Kuzikana* Walibora anasema:

Tom alikuwa **anafanya kazi na shirika moja lisilo la serikali liitwalo Anken. Alikuwa anaishi mtaa wa Milimani, kama mjomba wake Tim.** Nilihofia kupata mapokezi kama yale niliyopata kwa mjomba wake Tim. Pamoja na umaarufu wake, sikuwa nimepata wasaa wa kutangamana na Tom niujue wasifu wake barabara. (*Kufa Kuzikana*, uk 81)

Mhusika Tom ambaye ni Mkanju anazo sifa nyingi. Ni msomi aliyekwenda Marekani kusoma akahitimu shahada ya uzamili, kisha akaoa mke mzungu.

Kando na kufanya kazi katika shirika la Anken, anaishi mtaa wa Milimani alikoishi mjombake Tim ambaye ni Mkorosho. Kinachodhihirika ni kwamba wanajamii wote kutoka tamaduni tofauti wanazo nafasi sawa za maisha pakiwemo elimu na nafasi za kazi. Kwa hivyo hakuna haja ya kuwepo na ubaguzi wa aina yoyote kwa misingi ya kikabila, jambo ambalo walibora katika *Kufa Kuzikana* anatumia kuonyesha jitihada za mshikamano wa kitaifa.

Kuhamasisha Jamii

Wamitila (2003) anaeleza fasihi kuwa sanaa ya lugha inayoshughulikia masuala yanayomhusu binadamu, matatizo yake, ndoto zake, matumaini yake, migogoro yake na jinsi anavyoingiliana na mazingira yake. Kwa msingi huu, Walibora ametumia wahusika katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* kuhamasisha jamii kuhusu athari za mizozo hasa kwa misingi ya kikabila. Dondoo lifuatalo linashadidia:

“...mheshimiwa sasa unaanza kuzungumza kama mtu aliyefunguka skrubu za akili. **Wakanju ni ndugu zetu ati.** Watu wa fikra kama zako ndio maharabu wa nchi.” (*Kufa Kuzikana*, uk 2)

Mwalimu Alex anamzomea mbunge Johnstone Mabende hadharani baada ya kutoa kauli za uchochezi katika hotuba yake. Licha ya kuwa Mwalimu Alex ni Mkorosho anawakumbusha wanajamii kuwa Wakanju ni ndugu zao na kuwa wanapaswa kuishi kama ndugu. Vilevile mhusika Tom anakashifu ukabila kwa kusema:

“...**Ukabila ndio ugonjwa mbaya, ul'oenea kote. Bora utafutiwe dawa,**”

Alitoa kauli Tom. “Dawa itoke wapi?” Tim aliuliza. “Kwanza swali hili. **Wewe kabila gani? Tuling'oe kwenye mazungumzo yetu.** Mtu akuulizapo ‘wewe kabila gani?’ anajaribu kupima masafa yanayoku tenga naye.” (*Kufa Kuzikana* uk, 90)

Kwa maoni ya Tom, ukabila ni ugonjwa ambao unapaswa kutafutiwa dawa, hasa kwa kuepuka kauli za kuuliza kabila la mtu katika mazungumzo. Kutokana na mifano iliyotolewa, Walibora anahamasisha jamii kuhusu athari za mizozo ya kikabila, ambayo hutishia mshikamano wa kitaifa.

Maono Sawa na Hisia za Umoja

Kutokana na mtazamo wa Walibora kuhusu mshikamano wa kitaifa, kuwepo kwa maono sawa na hisia za umoja miongoni mwa wanajamii huchangia pakubwa Katika kuleta mshikamano huo. Dondoo lifuatalo linathibitisha:

...Ee! Bwana,” alidakia maneno Tim. “Watu wa taifa hili husahau kuwa

sote ni ndugu, asili yetu shamba la Edeni. Sote njia yetu moja. hakuna tofauti baina ya mtu wa kabila hili wala lile.” (*Kufa Kuzikana*, uk 90)

Mhusika Tim anawakumbusha Akida na Tom kuwa watu wote ni ndugu kwa kuwa asili yao ni moja, na kuwa hatimaye njia yao ni moja, jambo ambalo anadai kuwa watu wa taifa la Kiwachema wamelisahau. Kwa kusema maneno hayo, Tim anaongozwa na misingi dhabiti ya kidini ambayo ni muhimu katika kusuluhisha mizozo na hatimaye kuleta msikamano katika taifa. Haya yanaafikiana na maoni ya Mworio na Ndiku (2012) kuhusu umuhimu wa dini katika kuhimiza amani na upendo miongoni mwa wanajamii kwa msingi kuwa watu wote ni ndugu na hatima yao ni moja, jambo ambalo Walibora katika *Kufa Kuzikana* anahimiza.

Kuthamini Tamaduni za watu Wengine

Katika *Kufa Kuzikana*, baadhi ya wahusika wamejitokeza kuwa wanathamini tamaduni za watu wengine katika jamii. Kwa mfano:

... “Ah! Jina langu si muhimu,” alisema hima huku anachekacheka.” Tangu nifike Kiwachema miaka mitatu iliyopita, **nimeona watoto na wanawake wakinasibishwa tu na baba na waume zao.** Mathalan kule Baraki Tom si Tom, ni mtoto wa Mangala nami si Janelle, ni mke wa mtoto wa Mangala na kadhalika. “...**lazima nizingatie mila ya watu wa Tom.**” (*Kufa Kuzikana*, uk 82-83)

Janelle ni mzungu kutoka Canada ambaye ni mke wa Tom. Baada ya kuhamia nchi ya Kiwachema alikozaliwa mumewe Tom, Janelle anajitambulisha kikamilifu na tamaduni na mila za Wakanju, kabila la Tom. Hii ndio maana anasema kuwa hata kujua jina lake si muhimu kwani miongoni mwa jamii ya wakanju watu wanajitambulisha na ukoo wao. Hali ya kuthamini na kuenzi tamaduni za watu wengine inajitokeza pia kupitia mfano ufuatao:

“Basi **kabila lake Msangura**, sio?? nikamwuliza. “Ndiyo, unajua tena Wakoloni walivyowapiga mafungu Wanakiwachema kwa kulipa kila kabila wilaya yake, na kila wilaya jina la kikabila. **Pam ni Msangura...**” ...tunapanga kwenda kuwaona wazazi, wake na wangu. **Tumeazimia kufunga ndoa** wala hatutetereki.”

Kutokana na dondoo lililotolewa, licha ya kuwa Tim ni Mkorosho, anamchumbia Pam ambaye ni Msangura. Hii inaonyesha kuwa maisha ya wahusika hawa hayathibitiwi na hisia za kikabila. Kwa hivyo Walibora anatoa mchango mkubwa katika mshikamano wa kitaifa kwa kuonyesha kuwa kuna uwezekano wa wanajamii katika taifa lolote lile kuishi na kufanya maamuzi muhimu yasiyotawaliwa na hisia za kikabila kwa vyovyote vile.

Changamoto za Mshikamano wa Kitaifa

Licha ya juhudi mbalimbali katika kuleta mshikamano wa kitaifa, Walibora anaonyesha kuwa kunazo changamoto nyingi katika harakati hizo. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

Tamaa na Ubinafsi

Tamaa na ubinafsi miongoni mwa wanajamii huwafanya kuwaonea wenzao gere, jambo ambalo linaweza kusababisha mizozo ya kijamii.

Katika *Kufa Kuzikana*, kifungu kifuatacho kinathibitisha:

“...Sasa Wakoroshu wanataka watutumie tuwaondokee Koroshu. Mara biashara yetu inaipiku yao, tuna uchawi. Mara kilimo chetu kina tija Zaidi, tunatumia usihiri. Mambo yetu yanatawasari mno. Yao yanakwenda kombo. Na sasa tuondokeje Koroshu, mahala tulipoishikwa vizazi vingi tangu mababu na mababu zetu. Na siri ya mafanikio yetu ni ari na bidii.” (*Kufa Kuzikana*, uk 75)

Sababu kuu ya kuzuka mizozo ya kikabila Wilayani Koroshu ni kutokana na wivu wa Wakoroshu kwa Wakanju kuhusu kuimarika kwa biashara zao, kilimo kunawiri na kutawasari kwa mambo yao. Kama anavyodai mhusika Mzee Uledi, siri ya mafanikio yao ni ari na bidii yao wala sio uchawi. Tamaa na ubinafsi wa Wakoroshu zinawafanya kuzua vurugu na kuwatimua Wakanju mahali pale. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, Wahusika ni vielelezo yakini vya binadamu wa kawaida kwa vile wao hutumia lugha ya binadamu wa kawaida. Hali halisi ya wahusika na lugha wanayoitumia humwezesha mwanadamu kujifafanulia uwezo wake wa kutenda mambo na mtazamo wake kuhusu maisha. Kwa msingi huu, Walibora ametumia wahusika Wakoroshu kuwakilisha wananchi katika mataifa mengi hasa nchini Kenya kama ilivyotendeka mwaka wa 1992 eneo la Bonde la Ufa kulipotokea mzozo katika mji wa Molo. Kimsingi, uhasama ulikuwa baina ya jamii za Wakalenjin na Wakikuyu ambapo umilikaji wa ardhi ulikuwa kichocheo mojawapo cha mzozo huo. Watu zaidi ya elfu tano waliuawa na wengine elfu sabini na tano wakaachwa bila makao.

Kuzorota kwa Maadili

Watu wenye maadili wana uwezo wa kutambua mambo sahihi na yasiyo sahihi. Aidha, maoni yao kuhusu maadili hayabadiliki kwa kutegemea hisia walizonazo wakati huo. Hata hivyo, kuzorota kwa maadili kunaweza kuvuruga mshikamano wa kitaifa. Kwa mfano:

“Nyie Wakanju ni wajinga,” “Ee Tamari” nilimaka, “Nyie ni wauaji,” aliendelea kufoka huku anacho kikombe cha chai mkononi, kaka kitandani. “...Nenda huko bwege wewe,” alinitupia tusi.

“Mwanzo unafanya nini katika nyumba ya kakaangu? (*Kufa Kuzikana*, uk 63)

Tamari anamrushia Akida cheche za matusi kwa kumwambia kuwa Wakanju ni wajinga na wauaji, jambo linalomkera sana Akida. Hii inadhihirisha hali ya kuzorota kwa maadili katika jamii, jambo ambalo ni changamoto katika mshikamano wa kitaifa.

Mielekeo hasi ya Kikabila

Kuna uhusiano wa karibu baina ya mielekeo ya wanajamii kuhusu makabila mengine na mshikamano wa kitaifa. Kwa mfano:

“Hakuna watu wajinga kama wakanju. Mimi huwa nasema kwa jahara mambo haya, sifichi kitu.” Maneno ya mzee yule yalinidunga moyoni kama upanga unaokatia makalini na nafutuni. “Hebu niambie kijana,” aliendelea. “Babako ana wake wangapi?...**hakuna mkanju ana mke mmoja tu. Number two, Wakanju wanapenda matanga sana,** (*Kufa Kuzikana*, uk 25-26)

Katika dondoo lililotolewa, mjombake Tim anamdhalilisha Akida hadharani kwa misingi ya kabila lake jambo ambalo Akida anakiri kuwa linamdunga moyoni kama upanga. Kwa mujibu wa Chachali (2008), ghasia za baada ya uchaguzi mkuu nchini Kenya mwaka 2007-2008 zilidhihirisha kuwa ukabila unaweza kuitumbukiza nchi katika vita. Kwa hivyo Walibora anatumia fasihi kuhamasisha jamii kuhusu haja ya kuwa na mielekeo chanya kuhusu makabila mengine ili kuepuka mizozo.

Hisia za Ubora miongoni mwa Wanajamii

Hisia za ubora miongoni mwa wanajamii ni mojawapo ya changamoto katika mshikamano wa kitaifa. Mfano ufuatao unathibitisha:

Muradi mjadala kuhusu makabila ya wachezaji na wakufunzi, wenye vipawa na wasio vipawa, ulipamba moto. Ndivyo vilivyokuwa vikao hivyo. **Hata kabila la mtangazaji lilikuwa suala nyeti. Anaweza kutangaza vyema au la kutegemea kabila lake,** si umilisi wake mwenyewe. (*Kufa Kuzikana* uk, 4)

Kutokana na dondoo lililotolewa, inathihirika kuwa watu katika jamii walipima uwezo wao kwa misingi ya kikabila. Mathalan ubora wa wachezaji au watangazaji ulitegemea kabila la mtu, wala si umilisi wake mwenyewe. Katika *Kufa Kuzikana*, Walibora analiweka jambo hili wazi ili kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kuthamini watu wote kama ndugu. Aidha, anakashifu mitazamo ya watu katika jamii ambapo baadhi yao hujihisi kuwa bora kuliko wengine, kwa kuonyesha kuwa kuna njia mbadala za kupima uwezo, umilisi na tajriba za watu wala si misingi ya kikabila.

HITIMISHO

Makala hii imejadili mchango wa Ken Walibora katika mshikamano wa kitaifa kwa kutathmini riwaya ya *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003). Dondoo zilizokuliwa na kuchanganuliwa zimethibitisha kuwa Walibora katika *Kufa Kuzikana* amerejelea chanzo cha mizozo katika jamii kama vile ukabila, siasa na masuala ya ardhi. Aidha, Walibora ameonyesha kuwa juhudi za wanajamii zinaweza kusaidia katika kuleta mshikamano wa kitaifa. kwa mfano, kuwepo na mahusiano dhabiti na bora, kuwa na nafasi sawa za maisha miongoni mwa watu kutoka tamaduni tofauti, kuhamasisha jamii, kuwa na maono sawa na hisia za umoja na hali ya kuthamini tamaduni za watu wengine. Hata hivyo, Walibora ameonyesha kuwa kunazo changamoto nyingi katika juhudi za kuleta mshikamano wa kitaifa. Changamoto hizo ni pamoja na tamaa na ubinafsi, kuzorota kwa maadili, mielekeo hasi ya kikabila na hisia za ubora miongoni mwa wanajamii. Kwa hivyo, imedhihirika kuwa fasihi hasa utanzu wa riwaya inaweza kuangazia masuala ya kijamii kama vile kuhamasisha na kuzindua jamii pana kuhusu umuhimu wa mshikamano wa kitaifa.

MAREJELEO

- Arthur, M. (1918). *Realism: A Study in Art and Thought*. London: Constable and Company Ltd.
- Government of Kenya. (2008). The National Cohesion and Integration Act No. 12 of 2008. Nairobi: Government printer.
- Hegel, G.W.F (1979). *Introduction to Aesthetics*. Oxford: Clarendon.
- Kimenyi, M. S & Ndung'u, S.N (2005). Sporadic Ethnic Violence: Why Has Kenya Not Experienced a Full-blown Civil War? In p/ Collier and N. Sambanis (Eds), *Understanding Civil War* (Vol. 1: Africa), World Bank: Washington D.C.
- Lukacs, G. (1963). *The Meaning of Contemporary Realism*. London: Merlin Publishers
- MoJNCCA (2012). *Uwiano na Utangamano wa Kitaifa; Mwongozo wa Mafunzo*. Nairobi: government printer.
- Muchiri, J. (2016). *The Burden of Tribal Clashes Lies Heavily on Kenyan's Hearts*. *Daily Nation* on 3rd July. Nairobi: Nation Media Group.
- Mworia, L & Ndiku, J. M. (2012). Inter Ethnic Conflict in Kenya: A Case of Tharaka-Tigania Conflict, Causes, Effects and Intervention Strategies. *Journal of Research in Peace, Gender and Development*. vol.2 (7) pp. 162-170, July 2012.
- Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.

- Nyanda, P.C. (2017). Umuhimu wa Mshikamano wa Kitaifa Kuboresha Maisha ya Binadamu Accessed at www.archivioradiovaticana.va/storico/2017/06/07/umuhimu_wa_mshikamano_wa_kimataifa_kuboresha_maisha_ya_binadamu/sw-1317468: on 24/07/2020.
- Nyiri, J.K (2014). The Impacts of Ethnic Conflict on Economic Development: The Case of Post-Election Violence in Kenya, 2007-2008. (M.A) Masters Project: University of Nairobi.
- Republic of Kenya. (2010). *Constitution of Kenya*. Nairobi: Government Printer.
- UN (2013). Umuhimu wa Mshikamano baina ya Binadamu Waangaziwa nchini Kenya. Accessed from: news.un.org/sw/story/2013/12/366832-umuhimu-wa-mshikamano-baina-ya-binadamu-waangaziwa-nchini-kenya. On 24/07/2020.
- Walibora, K. (2003). *Kufa Kuzikana*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Limited.
- Wellek, R. & Warren, A. (1954). *Theory of Literature*. London: Harcourt, Brace, and Company.